



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

TAARIFA KWA UMMA

MWALIKO WA WATAZAMAJI WA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA SIHA NA KINONDONI NA UDIWANI KATIKA KATA 9 KWENYE HALMASHAURI ZA TANZANIA BARA

Kwa mujibu wa kifungu cha 46 (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 48 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Majimbo mawili na Kata tisa. Uchaguzi huo utafanyika tarehe 17 Februari, 2018. Orodha ya majimbo na Kata zenye uchaguzi ni kama ifuatavyo:.

Majimbo yatakayofanya Uchaguzi Mdogo ni:-

Na	MKOA	JIMBO	HALMASHAURI
1.	KILIMANJARO	Siha	Halmashauri ya Wilaya ya Siha
2.	DAR ES SALAAM	Kinondoni	Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni

Kata zitakazofanya uchaguzi mdogo.

Na	MKOA	HALMASHAURI	NA.	KATA
1.	MWANZA	Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana	1.	Isamilo
2.	DODOMA	Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino	2.	Manzase
3.	TANGA	Halmashauri ya Wilaya ya Pangani	3.	Madanga
4.	KAGERA	Halmashauri ya Wilaya ya Muleba	4.	Buhangaza
5.	MWANZA	Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi	5.	Kanyeleele
6.	SINGIDA	Halmashauri ya Manispaa ya Singida	6.	Mitunduruni

Na	MKOA	HALMASHAURI	NA.	KATA
7.	KILIMANJARO	Halmashauri ya Wilaya ya Siha	7.	Kashashi
			8	Gararagua
			9	Donyomuruak

Kwa ajili ya kuweka uwazi katika Uchaguzi huo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia Kanuni ya 18 (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge 2015, inapenda kualika Asasi za Kiraia na Taasisi mbalimbali za ndani zinazotaka kuwa Watazamaji wa Uchaguzi katika Uchaguzi Mdogo unaotarajiwa kufanyika tarehe 17 Februari, 2018.

Asasi/Taasisi zinapaswa kuzingatia masharti yafuatayo wakati wa kuwasilisha maombi yao:-

- (i) Anuani Kamili ya Taasisi husika,
- (ii) Anuani ya Makazi ya Ofisi ya Taasisi husika ilipo,
- (iii) Mahali /Sehemu ambapo Taasisi husika inafanya kazi.
- (iv) Shughuli ambazo zinafanywa na Taasisi husika kwa mujibu wa Hati ya Usajili.
- (v) Kutaja sehemu ambazo Asasi/Taasisi inataka kufanya zoezi hilo la Utazamaji.
- (vi) Kutaja idadi ya watu ambao Taasisi / Asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na taarifa zao.
- (vii) Kutaja majina na namba za simu za viongozi wa Taasisi husika kama yalivyoandikwa katika Hati za Usajili wa Taasisi.
- (viii) Ikiwa Taasisi inahusisha Watendaji wa Kimataifa, wawili lazima wawe watanzania.
- (ix) Kuambatanisha nakala/kivuli cha hati ya Usajili wa Taasisi husika.
- (x) Kuambatanisha nakala / kivuli cha Katiba ya Taasisi / Asasi husika.

Vilevile, Taasisi zitakazopewa vibali vya kuwa Watazamaji zitapaswa kuzingatia Mwongozo kwa watazamaji wa ndani na wa Kimataifa ulioandaliwa na Tume kwa

mujibu wa Kanuni ya 24 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2015na Kanuni ya 20 ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani za mwaka 2015.

Maombi ya kuwa Watazamaji wa Uchaguzi yatapaswa kuwasilishwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Makao Makuu si zaidi ya tarehe 10 Februari, 2018 kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Posta House, Ghorofa ya 7,
Mtaa wa Ghana/Ohio,
S. L. P. 10923,

DAR ES SALAAM.

Imetolewa leo tarehe 26 Januari, 2018, na


Kailima, R.K.
MKURUGENZI WA UCHAGUZI